

# ILANI YA UCHAGUZI YA WANAWAKE

## UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA WA 2024 NA UCHAGUZI MKUU WA 2025

*Ajenda ya Mwanamke, Turufu ya Ushindi*

TGNP

MTANDAO WA WANAWAKE NA KATIBA

WOMEN FUND TANZANIA
Empowering Local Women Heroes

# ILANI YA UCHAGUZI YA WANAWAKE

## UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA WA 2024 NA UCHAGUZI MKUU WA 2025

*Ajenda ya Mwanamke, Turufu ya Ushindi*



# 1.0 UTANGULIZI

Ilani hii inaendeleza madai ya wanawake watetezi wa haki za ushiriki katika uongozi wa kisiasa tangu tupate uhuru hadi leo. Ilani hii ni ya sita iliyobeba madai yetu rasmi tukiwa wadau na washiriki wakuu katika michakato mbalimbali ya uchaguzi. Ilani ya kwanza ilikuwa ya mwaka 2000 ikijulikana kama Ilani ya Wapigakura, ya pili ni ya mwaka 2005, ya tatu ni ya mwaka 2010, ya nne ni ya mwaka 2015 ya tano ni ya mwaka 2020. Maandalizi ya ilani zote sita yaliongozwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kwa kupitia Mtandao wa Wanawake na Katiba, Uchaguzi na Uongozi unaoratibiwa na Mfuko wa Ufadhili wa Wanawake Tanzania (WFT_T) pamoja na mitandao mingine ya Tapo la Ukombozi wa Wanawake Kimapinduzi. Masuala nyeti yaliyodaiwa katika Ilani zilizopita pamoja na kuibuliwa wakati wa mchakato wa katiba mpya ni pamoja na:

a) Kukosekana kwa utashi wa siasa katika kuleta mabadiliko ya mifumo kandamizi ikiwa ni pamoja na mfumodume

b) Licha ya kufanikiwa kuwa na Rais mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huu tangu tupate uhuru, hatujaona mabadiliko makubwa kwenye ngazi nyingine za maamuzi.

c) Chaguzi zisizokuwa huru na za haki kwa mtazamo wa kijinsia.

d) Mwendelezo wa sheria, sera na mipango isiyozingatia mrengo wa jinsia: Sheria hizi ni pamoja na sheria za uchaguzi, sheria ya ndoa inayohalalisha ndoa za utotoni, sheria ya vyama vya siasa isiyowajibisha vyama kuzingatia usawa wa jinsia katika uongozi wa vyama na uteuzi wa wagombea

e) Ukatili dhidi ya wanawake na watoto wa kike.

f) Kukosekana kwa uwajibikaji katika utekelezwaji wa misingi ya usawa wa jinsia kama iliyoainishwa kwenye mikataba ya kimataifa, kikanda, katiba ya nchi pamoja na Dira ya Taifa 2025.

g) Kwetu sisi Wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozi, masuala yaliyoibuliwa katika Ilani zilizopita pamoja na yale tuliobainisha wakati wa mchakato wa kutayarisha Katiba Mpya na kuingizwa kwenye Katiba inayopendekezwa ya Oktoba 2014, bado tunaona mafanikio madogo sana kwenye ngazi nyingi za uongozi, na kwamba mfumo dume unazidi kujiimarisha katika nyanja mbalimbali na kwa kutumia mikakati mbalimbali.

## 1.1 Sisi ni Nani?

Ilani hii imejumuisha sauti za Wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozi wenye takribani asasi za kiraia 175 kutoka ngazi ya kijamii, kitaifa, Mtandao wa Wanawake na Maji, Mtandao wa Bajeti yenye Mrengo wa Jinsia, Wanaharakati wa Tapo la Ufeminia, na Vituo vya Taarifa na Maarifa. Ilani hii inaendeleza madai yetu tukiwa watanzania, wapiga kura, na wanaharakati wa haki za binadamu hususani haki za wanawake za kushiriki katika maamuzi yanayohusu maendeleo yetu na ya nchi yetu. Mtandao huu uliundwa na kuimarika wakati Serikali ya Awamu ya Nne ilipoamua kuanzisha mchakato wa kutayarisha katiba mpya. Kwa sauti moja tuliweza kuingiza masuala 11 kati ya masuala 12 tuliyobainisha kwenye Katiba iliyopendekezwa. Mchakato huu ulipoahirishwa na awamu hiyo hiyo, mtandao uliamua kujikita zaidi katika kudai ushiriki wa wanawake katika uongozi na maboresho ya sheria za uchaguzi ili kuondoa vikwazo vya kisheria vinavyohalalisha ubaguzi wa kijinsia katika uchaguzi.

Sisi Wanawake, Wanamtandao wa Katiba, Uchaguzi na Uongozi na wana tapo wengine wa Ukombozi wa Wanawake Kimapinduzi, tunatambua kwamba sisi ni wadau wakubwa katika chaguzi zote, kwanza tukitambua kwamba wanawake ni asilimia 51 ya watanzania wote, na kwamba ni asilimia kubwa ya wapiga kura, na tukiwa wanachama wa vyama vya siasa, na kwa kutambua umuhimu wa michango yetu katika kushiriki katika nafasi mbalimbali za uongozi wa nchi yetu katika ngazi zote, tunadai kwa pamoja kuwekwa kwa mazingira wezeshi ya ushiriki wetu katika ujenzi wa demokrasia ya kweli ikiwa ni pamoja na ushiriki wetu katika chaguzi zote mbili.

Kwa kutambua kwamba, nchi yetu imeridhia mikataba, itifaki na matamko na makubaliano mbalimbali ya kimataifa na kikanda yanayobainisha haki za wanawake katika uongozi, na ushiriki wetu katika ujenzi wa demokrasia halisi kwa njia ya chaguzi, kwa pamoja tunadai uzingatiaji wa mikataba na makubaliano haya ambayo nchi yetu imeridhia. Mikataba hii ni pamoja na Tamko la Kimataifa kuhusu Haki za Binadamu (UDHR : 1948), Mkataba wa Kimataifa kuhusu haki za wanawake katika siasa (U.N.T.S.135, (1954), Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza Aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW : 1979 Kifungu cha 7: a, b, na C), Mapendekezo ya Baraza la Usalama (UNSC 1325(2000), Mpangokazi wa Beijing (1995) Malengo ya Kimataifa ya Maendceleo Endelevu (SDG) hususan lengo la tano, Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu ikiwa ni pamoja na Mkataba wa Ziada wa Maputo. Haki za ushiriki wa wanawake katika siasa na uongozi zimebainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977). Vilevile, azma ya kutokomeza aina zote za ubaguzi imebainishwa katika Dira ya Taifa (2025) pamoja na sera na mikakati mbalimbali. Aidha, vyama vingi vya siasa hapa nchini vimeingiza kwenye katiba au sera zao dhamira ya kujenga demokrasia ya kweli kwa njia ya kuondoa vizingiti

vinavyokwamisha wanawake kushiriki katika nyanja mbalimbali za uongozi.

Kimantiki, sisi tunasema kwa sauti moja kwamba, hapajakuwepo na utashi wa kisiasa wa kubomoa misingi inayokwamisha wanawake kwenye ushiriki wao kama raia huru katika chaguzi zote zilizopita.

## 1.2 Ilani hii Inamlenga Nani?

Walengwa wa kwanza ni sisi wanawake ambao ni wapiga kura, wenye nia na haki ya kushiriki katika uchaguzi, na hatimaye kushiriki katika kuliongoza taifa letu kwenye maeneo mbalimbali. Ilani hii ni wito kwetu sisi wanawake wote kuungana na kupaza sauti kwa pamoja tukiwa na ajenda moja ya kudai mabadiliko ya mfumo/mifumo kandamizi na yenye kutubagua. Kwa sauti moja tunasema, hatuwezi kujenga demokrasia thabiti kama chaguzi zetu si huru na za haki kwa mtazamo wa jinsia.

Vilevile, Ilani hii inailenga serikali iliyoko madarakani, tukiitaka serikali, taasisi na vyombo vyote vinavyohusika na uchaguzi viwajibike kuzingatia mikataba, itifaki, matamko ya kimataifa na kikanda pamoja na misingi ya kikatiba iliyoainishwa kwenye dira ya taifa 2025, kuchukua hatua za makusudi ili kuondoa vikwazo vinavyoendeleza ubaguzi katika ushiriki wetu katika uchaguzi kama wapiga kura, au wagombea wanaowania nafasi mbalimbali za ushindani na hatimaye, kustahili kushiriki katika uongozi katika nyanja mbalimbali za jamii yetu. Ilani inatoa wito kwa serikali iliyoko madarakani kuchukua hatua za makusudi za kusawazisha mazingira ya uchaguzi ili wanawake waweze kushiriki bila vikwazo vinavyowabagua. Ni ilani inayotoa wito kwa serikali iliyoko madarakani kuelekeza matumizi ya rasilimali za uchaguzi ili kuwanufaisha wagombea wanawake na wanaume, na kusimamia mchakato wote wa uchaguzi ili kuwezesha kuwa na uchaguzi huru na wa haki kwa mrengo wa jinsia.

Ilani hii inavilenga vyama vya siasa, ambavyo katika muktadha wa uchaguzi, vina uwezo mkubwa wa kuamua ni nani aingie kwenye kinyang'anyiro cha uchaguzi, ni nani afungiwe milango na ni nani aungwe mkono hadi hatua za ushindi. Ilani inalenga kuhamasisha vyama hivi vione faida ya kufungua milango kwa wanawake ili kujenga demokrasia thabiti ndani ya vyama vyao. Pamoja na kuvionesha nguvu ya kura zetu kwenye uamuzi wa mwisho kuhusu nani tutakaeyempa dhamana ya kuongoza taifa letu kwa kipindi cha miaka mingine mitano.

Ilani inalenga vyombo vya Habari, kutokana na nguvu ya vyombo hivi kuleta mabadiliko ya mtazamo kuhusu nafasi ya mwanamke katika uongozi wa taifa hili.

Vilevile, ilani inalenga wapiga kura wote na hasa wanawake, kutokubali kununuliwa au kudanganywa kuuza kura zao kwa wenye uchu wa madaraka, ambao hawana nia ya kuwakilisha sauti zao, na hasa kwa wanawake na vijana, ilani inawahamasisha kukataa kurubuniwa kwa maneno au kwa vitu vitakavyowapokonya haki yao ya msingi ya kushiriki kwenye mchakato wote wa uchaguzi.

Mwisho, lakini si kwa umuhimu, Ilani inalenga serikali tutakayoipa dhamana kwa kupitia kura zetu iwajibike kutekeza na kuchukua hatua stahiki ili kuifikia dira ya taifa ya kufanya ubaguzi wa aina yoyote ikiwa ni pamoja na kutokomeza ubaguzi wa kijnsia. Hivyo basi, ILani hii ina malengo yafuatayo:

## 1.3. Malengo ya Ilani

Lengo kuu la Ilani hii ni kudai mabadiliko ya mifumo kandamizi inayohalalisha ubuguzi wa wanawake katika uchaguzi kama wapiga kura, wenye kuwania nafasi za teuzi na hatimaye kuwakwamisha kwenye kuchaguliwa kama wawakilishi katika ngazi mbalimbali. Sisi wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi na wanatapo wengine kwa pamoja tunatambua vikwazo vilivyo kwenye muktadha wetu, na pia tunaelewa fursa zilizo wezeshi endapo kutakuwa na utashi wa kisiasa ndani ya jamii zetu, ndani ya vyama vyetu na ndani ya uongozi wetu wa kuleta mbadiliko makubwa katika mifumo yote kandamizi ikiwa ni pamoja na mfumo wa uchaguzi. Kwa mantiki hii, madhumuni mahususi ya Ilani hii ni pamoja na:

### 1.3.1 Madhumuni Mahususi:

- Kuchambua muktadha wa siasa, uchumi na ustawi wa jamii ili kuelekeza madai yetu yatokanayo na muktadha huu.
- Kuweka bayana madai yetu ya chaguzi hizi mbili za mwaka 2024 (Serikali za mitaa) na 2025, (Uchaguzi Mkuu) kwa wadau wote husika
- Kuainisha changamoto zitokanazo na mfumo wa utandawazi, ubepari, Ubeberu na mfumodume unaowapendelea na kuwapa fursa na mamlaka zaidi wanaume na kukwamisha harakati za ukombozi wa wanawake kimapinduzi.
- Kuchanganua haki na wajibu wa wadau mbalimbali katika chaguzi tajwa
- Kuhimiza kuwekwa kwa mifumo mbadala ya uwajibikaji katika ngazi zote; Serikali za Mitaa, Madiwani, Wabunge, Baraza la Mawaziri, Bunge na Serikali Kuu.

- Kupendekeza mikakati endelevu ya kuwahamasisha wapigakura wote, hususani wanawake katika kuweka nguvu zao za pamoja ili kudai yale ambayo wanayawekea kipaumbele na kusimamia utekelezaji wa ahadi za wale wote tutakaowapa dhamana kuliongoza taifa letu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

## 2.0 Muktadha

Sehemu hii ya Ilani, itajikita katika uchambuzi wa muktadha wa kimataifa na wa kitaifa kama ifuatavyo.

### 2.1 Muktadha Kimataifa

Katika kipindi hiki cha miaka mitano hadi sita iliyopita, tulishuhudia kuimarika kwa itikadi za kiliberali, zilizoimarishwa na soko huria, kukua kwa matabaka ya uchumi kwenye pato la dunia na utajiri wa dunia. Kipindi hiki hiki dunia ilikumbwa na janga la UVIKO-19, lililogusa kila pembe ya dunia, maskini, na matajiri, lakini lililombebesha mwanamke mzigo wa ziada kwenye shughuli za uzalishaji na kuendeleza kizazi. Vilevile, kipindi hiki tumeshuhudia amani ya dunia ikitikiswa kutokana na mataifa makubwa kuchukua fursa za uhitaji wa silaha kuendeleza vita na migogoro katika mataifa mbalimbali duniani. Kwa mfano, vita huko Gaza, (vita vya Israel dhidi ya Palestina) vita vya Urusi dhidi ya Ukraini, machafuko katika bara letu la Afrika, huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kameruni, Bukinafaso, Mali, Ethiopia na Sudani Kusini. Hali ya vita imeathiri uhakika wa chakula, upatikanaji wa nishati, na mfumuko wa bei jambo ambalo linaendeleza kuongezeka kwa matabaka ya uchumi, afya, elimu na jinsia. Wanawake wanaendelea kubeba mzigo mkubwa zaidi kutokana na athari za vita, mfumuko wa bei na janga la UVIKO-19. Vilevile, mabadiliko ya tabianchi yanaendelea kuzibebesha nchi maskini mzigo mkubwa wa gharama zitokanazo na mabadiliko hayo, ambapo

wanawake wanabeba mzigo mkubwa zaidi katika upatikanaji wa nishati, hususani kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, uhaba wa maji, na athari kwenye kilimo na mifugo. Muktadha huu umeongeza mapengo katika maeneo haya:

### 2.1.1 Pengo la Pato na Utajiri Kimataifa

Ripoti ya Kimataifa ya Pengo (Inequality Global report 2022) inaeleza

a) Asilimia 10 ya matajiri wa dunia wanapata takribani asilimia 52 ya pato la dunia ambapo nusu ya maskini wote duniani wanapata asilimia 8.5 tu ya pato hilo.

b) Vilevile, ripoti hiyo hiyo imebaini kwamba pengo katika umiliki wa utajiri wa dunia ni kubwa zaidi. Takribani nusu ya maskini wote duniani wanamiliki asilimia 2 ya utajiri wa dunia, ambapo asili mia 10 ya matajiri wa dunia wanamiliki asilimia 76 ya utajiri wote wa dunia.

c) Ripoti hii inaeleza kwamba mapengo ya pato na utajiri yamekuwa yakiongezeka tangu miaka ya 1980 kutokana na mifumo inayoongozwa na itikadi za kiliberali.

d) Janga la UVIKO-19 limeongeza pengo katika umiliki wa utajiri, huku nchi zinazoendelea zikikumbana na changamoto nyingi za kukabiliana na janga hili pamoja na jitihada za kujinasua kiuchumi.

e) Vilevile, nchi maskini ambazo hazikuchangia sana katika mabadiliko ya tabianchi zimeendelea kubebeshwa mzigo mkubwa kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

f) Pengo la uchumi linaingiliana na mapengo mengine ikiwa ni pamoja na usawa wa jinsia, hali ya ulemavu, pamoja na hali ya kitabaka.

### 2.1.2 Pengo la Jinsia (kimataifa)

Katika muktadha huu, ripoti ya pengo la utajiri inasema kwamba, wanawake wanabeba mzigo mkubwa zaidi wa umaskini wakiwa na kipato cha asilimia 24 tu ikilinganishwa na wanaume, na inakadiriwa kwamba itaichukua dunia takribani miaka 170 kuziba pengo la kipato. Na kwamba zaidi ya asilimia 75 ya wanawake wote duniani wako kwenye sekta isiyo rasmi na kwenye kazi hatarishi zaidi ikiwa ni zile ambazo hazina malipo ya kujikimu. Jitihada za kuziba mapengo ya jinsia katika nyanja mbalimbali kimataifa, zimeonesha mafaniko madogo sana katika nyanja ya siasa. Ripoti ya Kimataifa (2022) kuhusu njaa imeonesha kwamba, takribani watu billion 3.1 hawawezi kumudu chakula chenye lishe bora na kwamba, takribani wanawake million 80 wanakabiliwa na njaa zaidi kuliko wanaume.

Kwa upande wa Bara la Afrika, ripoti ya Umoja wa Mataifa kuhusu hali ya Uchumi inaeleza kwamba bara la Afrika linakabiliwa na hali mbaya zaidi ya uhakika wa chakula ikiwa takribani asilimia 26 ya watu wake wana changamoto ya uhakika wa chakula. Wanawake wanabeba mzigo mkubwa zaidi utokanao na hali mbaya ya uhakika wa chakula kwa vile:

a) Changamoto itokanayo na mgawanyo wa kazi ndani ya kaya wakiwa wanatumia saa nyingi zaidi katika kuendeleza kaya kuliko wanaume
b) Wanawake wengi hawamiliki mali ikiwa ni pamoja na ardhi
c) Kipato chao ni kidogo zaidi kuliko wanaume kutokana na mifumo kandamizi inayowakwamisha kwenye kufikia huduma za kifedha na rasilimali (https://www.fao.org/3/cc0639en)

## 2.2 Muktadha wa Kitaifa

Tangu miaka ya 1980, nchi ya Tanzania ikishinikizwa na nchi za kibepari kwa kuongozwa na Benki ya Dunia na Mfuko wa Fedha Duniani, imekuwa ikitekeleza mfumo wa kiliberali, unaokinzana na falsafa ya uchumi linganifu, kujitegemea na ukombozi wa wanawake kimapinduzi. Mfumo huu wa Kiliberali umesisitiza ubinafisishaji wa njia kuu za uchumi pamoja na zile zinazotoa huduma kwa jamii kama vile afya, elimu, maji na usafiri. Mfumo huu umesababisha athari nyingi kwa uchumi na kuongeza mapengo kati ya wamiliki wa uchumi na wavuja jasho, wanawake wakiathirika zaidi katika nyanja nyingi. Mfumo huu umeathiri kwa kiasi kikubwa kuweko kwa mapengo ya jinsi katika uchumi, ustawi wa jamii, ushiriki katika uongozi na kuendeleza sera za ubaguzi.

### 2.2.1. Haki za Wanawake katika Uchumi

Kwa kipindi cha takribani miaka kumi iliyopita, uchumi wa Tanzania ulikua haraka sana na kufikia pato la taifa kwenye wastani wa asilimia 6-7. Katika kipindi hiki Tanzania ilikuwa miongoni mwa nchi 20 za Kusini mwa Bara la Afrika ambazo uchumi wake ulikuwa unakua kwa wastani wa asilimia 6-7 ukilinganisha na wastani wa asilimia 4.4 wa nchi nyingine kutoka bara hili, (https://www.tanzaniainvest.com/economy).

Hata hivyo, ongezeko la pato la taifa halikuwa na linganifu na vilevile halikuleta mabadiliko makubwa katika kupunguza umaskini. Kwa mfano, takwimu zinaonesha kwamba, kwa mwaka 2022, takribani watu million 26 Tanzania walikuwa kwenye umaskini wa kupindukia na kwamba mwaka 2021 takribani watu 100,000 waliingia kwenye umaskini wa kupindukia ukisababishwa na janga la UVIKO-19.

Sekta zilizokua kwa kasi ni zile ambazo hazitoi ajira kwa wingi na hasa kwa wanawake. Kwa mfano sekta ya ujenzi inaajiri asilimia 2.1 tu ya

watu wote, huku wanawake wakiwa ni asilimia 3 ya waajiriwa wote. Mawasiliano na Uchukuzi (TEHAMA) inaajiri asilimia 2.8 ya ajira zote ambapo kati yao, wanawake ni asilimia 5 tu. Sekta za huduma: afya, elimu na utumishi wa umma zinaajiri asilimia 3.9 tu ya ajira zote huku kati ya hao wanawake wakiwa asilimia 27 tu. Migodi inaajiri asilimia 1.1 ya waajiriwa wote, ambapo kati ya hao, wanawake ni asilimia 20 tu (Bodi za Takwimu Tanzania: Utafiti wa Bajeti ya Kaya: 2018)

Sekta ya kilimo ambayo inatoa ajira nyingi kwa wanawake ikitoa ajira kwa asilimia 69.9 ya wanawake dhidi ya asilimia 64.0 kwa wanaume. Takribani asilimia 34.5 ya wafanyakazi wote kwenye kilimo ni wale walioko kwenye shughuli zisizo na malipo wengi wao wakiwa wanawake. Sekta hii ilikua kidogo sana kwa asilimia 4 tu. (https://www.worldbank.org/en/country/tanzania/overview).

### 2.2.2 Usawa ya Jinsia katika Ajira

Katika ajira, tafiti zinaonesha kwamba jitihada za kuongeza ajira zimezaa matunda kwa kiasi kidogo sana. Idadi ya watu wasio na ajira imeshuka kutoka asilimia10.5 mwaka 2020 hadi asilimia 9.3 mwaka 2020/2021. Kwa wanawake wanaoishi vijijini, ukosefu wa ajira uliongezeka kidogo sana kutoka asilimia 9 mwaka 2014 hadi asilimia 9.6 mwaka 2020/2021. (https://www.repoa.or.tz/wp-content/uploads/2023/03/PB-01-Feb-2023-Gender-Balance).

Takwimu rasmi zinaonesha kwamba wanawake walioajiriwa kwenye sekta ya kilimo, wengi wao wako kwenye ajira isiyo na malipo, yaani kilimo cha kuhudumia familia na jamii. Mchanganuo wa ajira kisekta kijinsia ni kama ifuatavyo:

a) Utumishi katika serekili kuu: wanawake asilimia 42 na wanaume asilimia 58

b) Mashirika ya umma asilimia 18 wanawake na asilimia 82 wanaume

c) Sekta binafsi asilimia 28 wanawake na asilimia 72 wanaume

d) Idadi ya wanawake walioajiriwa katika sekta ya kilimo ikijumuisha kilimo, uvuvi na misitu imepungua kutoka asilimia 69 mwaka 2014 hadi asilimia 60 mwaka 2020/2021

e) Takwimu zinaonesha kwamba, ukosefu wa ajira kwa wanawake umeongezeka kutoka asilimia 3.6 hadi asilimia 16 kwa wale wanaoishi mijini na kwa wanaoishi vijijini kutoka asilimia 9 hadi asilimia 9.6 katika kipindi cha kutoka mwaka 2014 hadi 2020/2021.

f) Vilevile, ajira mpya hususani kwa vijana zilipungua sana huku changamoto ikiwa kubwa zaidi kwa vijana wa kike.

Pamoja na pengo kwenye ajira, taarifa rasmi zinaonesha kwamba, wanawake wengi wako kwenye ajira zenye kipato kidogo kuliko wanaume, na kwamba wafanyakazi wanawake wenye kipato chini ya Shilingi za Kitanzania 100,000 kwa mwezi ni asilimia 8.6 ukilinganisha na asilimia 6.5 ya wanaume wenye kipato hiki. Hata hivyo, asilimia kubwa zaidi ya wanaume wenye mshahara ya mwezi wa TSh 1,500,000 ni asilimi 5.6 ikilinganishwa na asilimia 4.4 ya wanawake.

### 2.2.3 Haki za Wanawake Kupata na Kunufaika na Huduma za Kifedha

Ripoti ya mwaka ya kutoka Mwongozo jumuishi wa taifa wa Kifedha (National Financial Inclusion Framework 2023-2028) inabaini kwamba, kumekuwa na jitihada za kuwezesha jamii ya Kitanzania kufikia huduma za kifedha kutoka asilimia 86 mwaka 2017 hadi asilimia 86 mwaka 2023. Hata hivyo pengo la jinsia bado lipo pamoja na kwamba pengo hili lilipungua kutoka asilimia 10 mwaka 2017 hadi asilimia 3.6 mwaka 2023. (https://www.bot.go.tz/Adverts/PressRelease/en/2023080516453703).

### 2.2.4 Haki za Wanawake katika Kumiliki Mali


Takribani asilimia 75 ya wanaume wana umiliki wa ardhi, ukilinganisha na asilimia 27 ya wanawake. Wanawake wenye umiliki wa ardhi wanalima mashamba madogomadogo zaidi na yenye kuzalisha mazao ya chakula cha kutosheleza mahitaji ya kaya. Mgawanyo wa kazi usio sawia huwapunja na kuwapotezea wanawake muda, jambo ambalo huathiri uwezo wao wa ushiriki kwenye kazi ambazo zingeweza kuwakomboa kutoka kwenye umaskini.

Kwenye umiliki wa nyumba takwimu zinaonesha kwamba asilimia 59 ya wanaume hawana umiliki wa nyumba ambapo asilimia 61.1 ya wanawake hawana umiliki wa nyumba. Vilevile, asilimia 25.6 ya wanaume wanamiliki nyumba wenyewe huku asilimia 7.4 tu ya wanawake wakimiliki nyumba wenyewe. Aidha, asilimia 7.9 tu ya wanaume humiliki nyumba na wenzi wao wakati wanawake wanaomiliki nyumba na wenzi wao ni asilimia 29.1. (https://genderdata.worldbank.org/countries/tanzania).


### 2.2.5 Haki za Wanawake Kupata na Kunufaika na Elimu

Katika ngazi zote za elimu, kuna pengo la jinsia kama takwimu kutoka Bodi ya Taifa ya Takwimu, zinavyoonesha

a) Kwa wale ambao hawajawahi kupata elimu kabisa, wanawake ni asilimia 22.3 ukilinganisha na asilimia 11.3 ya wanaume.





b) Asilimia 59 ya wanawake walifikia elimu ya msingi ukilinganisha na asilimia 63.7 ya wanaume




c) Asilimia 2.2 ya wanawake wamefikia elimu ya ufundi ukilinganisha na asilimia 3.8 ya wanaume. Ni asilimia 1.5 ya wanawake waliopata elimu ya juu kwenye vyuo vya kati ukilinganisha na asilimia 2 ya wanaume



d) Ni asilimia 0.8 tu ya wanawake wamefikia elimu ya shahada ukilinganisha na asilimia 1.9 ya wanaume




e) Pengo la jinsia katika ufikiaji wa elimu umezalisha pengo la jinsia katika ajira, hususani ajira zenye kipato cha juu.

f) Karibia kila mwaka idadi ya watoto wa kike wanaositisha masomo yao kutokana na mimba za utotoni ni kati ya 5,000 na 8,000.




(https://genderdata.worldbank.org/countries/tanzania) /

### 2.2.6 Haki za Wanawake Kupata na Kunufaika na Huduma za Afya

Pengo la jinsia katika huduma za afya linatokana na sababu nyingi, ikiwa ni pamoja na pengo la jinsia katika kunufaika na rasilimali za taifa, kiwango cha elimu, mifumo ya kibaguzi na hata hali ya ulemavu. Katika kufikia huduma za afya, mapengo yako kwenye maeneo haya:

a) Takribani asilimia 20 ya wanawake hujifungulia nje ya huduma rasmi za afya, jambo linalohatarisha maisha yao.

b) Asilimia 27 ya wanawake wenye umri kati ya 15 hadi 19, wana watoto, au ni wajawazito. Hii inamaanisha kwamba takribani asilimia 27 ya wasichana wa umri wa kwenda shule hawako shuleni au wamesitisha masamo yao, jambo linalowatumbukiza kwenye wimbi la umaskini na ufukara.

c) Takwimu za hivi karibuni zinabainisha kwamba, kati ya wanawake 238 kwenye kila wanawake 100,000 hufariki wakati wa kujifungua kutokana na sababu zinazoweza kuzuilika.

### 2.2.7 Haki za Wanawake na Upatikanaji wa Nishati

Hali ya upatikanaji wa nishati kwa ajili ya matumizi ya nyumbani imeendelea kuwa changamoto, kwani asilimia 85 ya kaya zote zinategemea kuni kama chanzo muhimu cha nishati kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Hali hii inambebesha wanamke mzigo mkubwa na kuathiri afya zao kutokana na ukweli kwamba wanawake ndio wanaowajibika zaidi katika kutafuta nishati kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Wanawake wanatembea kwa wastani wa kilometa 4 hadi 8 kutafuta kuni na kutumia takribani saa 4 hadi 5 kwa kazi hiyo. Hii inaathiri ubora wa maisha yao wenyewe na wakazi wa kaya husika.

Kwa kiwango kikubwa mapengo ya jinsia katika kuumiliki mali, ajira, elimu katika muktadha wa mifumo kandamizi vinaathiri ushiriki wa wanawake katika nyanja mbalimbali za uongozi.

### 2.2.8 Haki za Wanawake Kushiriki katika Nafasi Mbalimbali za Uongozi

Sisi wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi na mitandao mingine ya Tapo la ukombozi wa Wanawake tuna sababu ya kusherehekea kuwapo kwa mwanamke wa kwanza katika nafasi ya Urais tangu tupate uhuru. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliyepata kiti hiki baada ya kufariki kwa aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli. Kuwapo kwa Rais mwanamke kulitokana na msingi uliyotumika katika kuteua mgombea mwenza, kwamba endapo mwanaume ni mgombea wa kiti cha Urais basi mwanamke ateuliwe kuwa mgombea mwenza, au kama mwanamke ndiye mgombea kiti hiki basi mgombea mwenza awe mwanaume. Dai hili lilitokana na madai yetu ya mkakati wa kupata asilimia 50/50 katika ngazi ya uongozi wa taifa.

Sisi Wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozi na mitandao mingine ya Tapo la Ukombozi wa Wanawake tunadai msingi huu utumike katika teuzi zote za wagombea wa nafasi mbalimbali katika chaguzi za mitaa 2024 na uchaguzi mkuu wa 2025.

Hata hivyo, uwepo wa Rais Mwanamke katika ngazi ya juu ya uongozi, ushiriki wa wanawake katika ngazi nyingine za uchaguzi haujabadilika sana. Kwa mfano,

a) Ubunge: kumekuwa na ongezeko kidogo kutoka asilimia 31 katika bunge la 2005-2010 kufikia asilimia 37 katika Bunge la 2010-2015, ambapo asilimia hizi hizi zilibakia katika bunge la 2015-2020.

b) Ongezeko la wabunge wanawake limetokana na kuwapo kwa viti maalumu. Dhamira ya kuwapo kwa viti maalumu ilikuwa ni

hatua ya dharura ya kusawazisha uwanja wa ushindani ili hatimaye wanawake waweze kujengewa mazingira wezeshi ya kushindania uwakalishi katika ngazi zote. Hata hivyo, mfumo huu unaendelea kutumika kama mfumo rasmi wa uwakilishi wa wanawake katika vyombo vya uwakilishi. Kwa mfano katika Bunge la 9, wanawake walioingia bungeni kwa mfumo wa viti maalumu walikuwa 75 kati ya wanawake 101 (sawa na asilimia 74.2) Katika bunge la kumi kiwango hiki kikaongezeka hadi kufikia asilimia 78.5, Bunge la 11 kiwango hiki kikaongezeka na kufikia asilimia 79.3. Kwa kipindi hicho, kiwango cha wanawake wabunge waliochaguliwa ama kiliongezeka kidogo sana au kubakia pale pale.

Sisi Wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozi pamoja na mitandao mingine ya Tapo la Ukombozi wa Wanawake, tunasema kwa sauti moja kwamba mfumo wa viti maalum umekiuka dhamira yake, umeingiza mfumo wa kujenga tabaka la wabunge wenye stahiki duni ukilinganisha na wale waliochaguliwa kwenye majimbo. Mfumo huu haukuenda sambamba na jitihada za kurekebisha dosari zilizoashiria kuwabagua wanawake katika chaguzi mbalimbali. Mfumo huu sharti ubadilike. Mapendekezo ya mabadiliko ya mfumo huu yamebainishwa katika Katiba Iliyopendekezwa na Bunge Maalumu: Katiba inayopendekezwa Oktoba 2014.

Idadi ya wanawake kwenye nafasi za uteuzi imekuwa ikibadilika mara kwa mara. Kwa mfano,

idadi ya wanawake walioteuliwa katika nafasi za uwaziri iliongezeka kutoka asilimia 20 katika kipindi cha miaka ya 2005-2010 hadi kufikia asilimia 36 katika kipindi cha 2014-2015, ambapo kiwango hiki kilishuka kufikia asilimia 17 mwaka 2016, na kushuka zaidi kufikia mia 13 mwaka 2020. Takwimu za hivi karibuni zinaonesha kwamba, kwenye nafasi

ya Naibu Mawaziri ni asilimia 22, Makatibu Wakuu ni asilimia 18, Makamishina ni asilimia 16%, Wakuu wa Mikoa asilimia 8, Wakuu wa Wilaya asilimia 15, Mabalozi asilimia 33, Majaji asilimia 39 (Ofisi ya Rais Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma: 2021) (Ijulikane kwamba asilimia hizi huenda zimekuwa zikibadilika sana kutokana na mabadiliko ya mara kwa mara kwenye tuezi hizi).

### 2.2.9 Usawa wa Jinsia kwenye Vyama vya Siasa

Vyama vya siasa katika mfumo wa Demokrasia ya vyama vingi ni taasisi muhimu ya kujenga, kulea na kuimarisha kada ya viongozi wa kisiasa. Vilevile, vyama vya siasa ni nguzo kuu ya utawala bora kwa mantiki ya kuiwajibisha serikali iliyoko madarakani kuzingatia utawala wa sheria, haki na uwazi. Vyama vya siasa vinapopewa dhamana ya kuingia katika vyombo vya uwakilishi vinahusika katika utunzi wa sheria na sera za nchi. Hii inamaanisha kwamba vyama hivi vina nguvu ya kuleta mabadiliko katika mifumo kandamizi kwa kutunga sheria zitakazobatilisha sheria kandamizi ikiwa ni pamoja na sheria zinazohalalisha ukandamizaji wa kijinsia.

Hata hivyo, hali halisi ya ushiriki wa wanawake katika uongozi wa vyama ni hairidhishi.

Bado vyama vingi vimeendeleza utamaduni wa mfumodume, unaoruhusu wanaume wachache kuhodhi madaraka kwa kuwabagua wanawake.

a) Takwimu za uongozi wa vyama vya siasa zilizokusanywa mwaka 2015/2017 zilionesha kwamba, vyama vingi havikuwa na wanawake katika ngazi nne kuu kwenye uongozi wao, ikiwa ni pamoja na: Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu.

b) Takwimu za (2015/2017) zinaonesha kwamba, kwenye nafasi ya uenyekiti wa vyama 19 vilivyokuwa na usajili, ni ACT_Wazalendo tu ndicho kilichokuwa na Mwenyekiti mwanamke ambaye hata hivyo, hakuwa msemaji Mkuu wa Chama. Msemaji Mkuu wa Chama hicho alibakia kuwa mwanamume, Mh. Zitto Kabwe. Kwa takwimu za sasa hivi, hali haijabadilika sana kwani ni vyama viwili tu vyenye wenyeviti wanawake navyo ni Chama cha Mapinduzi (CCM) na Suti ya Umma (SAU).

c) Takwimu za 2015 zinaonesha kuwapo kwa wanawake wanne tu (asilimia 11) walioshika nafasi za makamu wenyeviti. Idadi hiyo imeongezeka hadi kufikia 10 kati ya nafasi 38 za vyeo hivi. Vyama hivyo ni: ACT_Wazalendo (bara), AFFP(bara), CCK (bara), DP(bara), UMD (Z'bar), ADA TADEA (bara), TLP (bara) NLD (bara), UPDP (bara), DP (bara).

d) Vilevile, katika kipindi hicho cha 2015/2017 kulikuwa na wanawake watatu tu (sawa na asilimia 16) walioshika nafasi ya Makatibu Wakuu wa vyama. Idadi hii imeshuka kufikia mwanamke mmoja tu aliyeshika wadhifa huo kwenye chama cha UDP kwa takwimu za 2022/2023.

e) Kwenye nafasi ya Naibu Katibu Wakuu, katika kipndi cha 2015/2017, kulikuwa na wanawake watano tu (sawa na asilimia 14) walioshika nafasi ya Naibu Katibu Mkuu, kati ya Naibu Makatibu Wakuu 37. Kwa kipindi hiki cha 2022/2023, idadi ya Naibu Makatibu Wakuu wanawake ni watano kutoka katika vyama vinne tuambavyo ni AAFP (Z'bar) CUF (Bara) NRA ((bara) na Demokrasia Makini (bara na Z'bar).

f) Taarifa ya Uongozi wa wanawake katika ngazi ya mikoa haikupatikana. Hata hivyo, chama tawala, CCM, kwa mwaka 2017, kilikuwa na viongozi wanawake wawili tu (sawa na asilimia 7) kutoka katika mikoa yote 30.

Licha ya ushiriki wao mdogo katika ngazi za uongozi, vyama vyote kuwategemea sana wanawake katika kunadi sera zao, kuwahamasisha wapiga kura kuchagua viongozi wao. Kwa mantiki hii:

Sisi Wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozi na mitandao mingine ya Tapo la ukombozi wa wanawake, tunakiri kwamba, vyama vingi havina mikakati ya kufungua milango kwa wanawake ili washiriki kikamilifu katika meza ya maamuzi ndani ya vyama husika. Vilevile hatuoni utashi wa kisiasa wa kubadilisha mfumo wa kibaguzi ndani ya vyama vyote vya siasa.

### 2.2.10 Ukatili Dhidi ya Wanawake

Ukatili dhidi ya wanawake na wasichana bado ni tatizo kubwa hapa kwetu Tanzania kwani ukatili huu hutumika kama njia ya kudhibiti na kukandamiza mwanamke na mtoto wa kike. Pomoja na kuwepo kwa jitihada mbalimbali za kutokomeza ukatili, bado takwimu zinaonesha kuendelea kwa tatizo hili. Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto Tanzania (2017/2018-2021/2022) ulibaini kwamba wanawake katika ngazi zote hupitia aina nyingi za ukatili ikiwa ni pamoja na kuumizwa kimwili, ukatili wa kisikolojia, ukatili wa kingono ikiwa ni pamoja na rushwa ya ngono. Takwimu za hivi karibuni zinaonesha kwamba:

a) Asilimia, 40 ya wanawake wenye umri kati ya miaka 15 hadi 49 wameumizwa kimwili, ambapo asilimia 17 wameumizwa kingono

b) Kati ya wanawake walio na umri kati ya miaka 15 hadi 49, asilimia 44 wameshapitia ukatili wa kingono na kimwili, mara nyingi na wenzi wao

c) Ukatili unaofanywa na watu wenye mahusiano ya karibu ni makubwa zaidi vijijini ambapo asilimia 52 wameshapitia kwenye ukatili ukilinganisha na mijini ambapo ni asilimia 45.

d) Karibu asilimia 30 ya washichana walio chini ya umri wa miaka 18 wameshaumizwa kingono.

e) Takwimu zilizokusanywa na Chama cha Waandishi wa Habari wa Wanawake (TAMWA) zilibainisha kwamba takribani asilimia 89 ya wanawake katika sekta binafsi wanadaiwa rushwa ya ngono kama sharti la kupandishwa cheo.

f) Vilevile, taarifa mbalimbali za wachunguzi wa chaguzi zilizopita zilionesha kuwapo kwa ukatili dhidi ya wanawake hususani wagombea wa nafasi mbalimbali. Hivyo basi,

Sisi Wanamtandao wa Wanawake Katiba, Uchaguzi na Uongozi na mitandao mingine ya Tapo la ukombozi wa wanawake, kwa sauti moja tunasema kwamba vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake ni njia mojawapo inayotumiwa kutoa ujumbe kwamba wanawake hawastahili kushika nafasi ya uongozi mahali popote kuanzia kwenye ngazi ya kaya. Ukatili huu sharti ukomeshwe.

Kutokana na uchambuzi huu uliobainisha mapengo ya jinsia katika nyanja mbalimbali za upatikanaji wa haki za wanawake, Sisi Wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozi na mitandao mingine ya Tapo la ukombozi wa wanawake, tumebainisha madai yetu hususani ya ushiriki wetu kwenye chaguzi hizi mbili, ule wa serikali za mitaa wa mwaka 2024 na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

## 3.0 Madai Yetu Katika Ilani

### 3.1. Madai kwa Serikali Iliyoko Madarakani

Serikali kwa kutumia idara na taasisi zake, ina jukumu kubwa la kusawazisha uwanja wa ushindani na hususani kuweka taratibu za kuwezesha kufikia lengo letu kuu la 50/50 kwenye uongozi wa taifa letu. Kwa mantiki hii, sisi Wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozi tukiwa raia wapiga kura, na watetezi wa haki za binadamu, na kwa kuzingatia haki za kimsingi kama zilivyoainishwa katika Mikataba mbalimbali ya Kimataifa na kikanda ambayo nchi yetu imeridhia, na kubainishwa kwenye Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dira ya Taifa ya 2025, pamoja na sera na mipango mbalimbali, tunasema kwa sauti moja, kwamba, wajibu wa serikali iliyoko madarakani ni kuweka mazingira rafiki na wezeshi ili wanawake washiriki kikamilifu kwenye chaguzi hizi bila vipingamizi vitokanavyo na mifumo ya kibaguzi ndani ya na nchi. Hii ni pamoja na maboresho ya sheria za uchaguzi, maboresho ya kanuni za uchaguzi kwa kuzingatia mapengo yaliyoainishwa katika Ilani hii. Jukumu la kuweka mazingira wezeshi kwa ushiriki wa wanawake litatekelezwa na taasisi, wizara na viongozi mbalimbali. Hivyo basi, sisi wapiga kura wanaharakati tunadai yafuatayo kwa serikali iliyoko madarakani kwa kupitia wizara na taasisi zake kama ifuatavyo:

### 3.2 Wizara ya Sheria na Katiba,

Wizara hii ikiongozwa na Tume ya Kurekebisha Sheria, iwajibike kufanya mapitio, utafiti na kutathmini sheria zenye upungufu unaoashiria kuhalalisha au kutoa mianya ya ubaguzi dhidi ya wanawake kwenye uchaguzi. Baadhi ya Sheria hizo ni:

a) Sheria ya Uchaguzi (CAP.343) (R.E.2015) ambayo haijakazia utekelezaji wa msingi ya usawa katika teuzi za wagombea

unaofanywa na vyama vya siasa bila vigezo vya uwazi, na uzingatiaji wa msingi wa usawa uliobainishwa kwenye sheria ya vyama vya siasa. Vilevile, kwenye suala la uwakilishi wa wanawake kwa kupitia mfumo wa Viti Maalumu vilivyoingiza misingi ya ubaguzi dhidi ya wanawake walioingia bungeni kwa mfumo huu. Wizara izingatie mapendekezo yetu kama ya mabadiliko ya mfumo huu kama yalivyoingizwa kwenye Katiba Iliyopendekezwa na Bunge Maalumu la Oktoba 2014.

b) Sheria ya Gharama za Uchaguzi (CAP 288 (R.E 2015) inayowabebesha wagombea wote mzigo wa gharama, bila kujali tofauti za kiuchumi kati ya wanawake na wanaume.

c) Sheria ya Vyama Vya Siasa (CAP 258 (RE 2015). Licha ya sheria husika kubainisha msingi wa usawa wa kijinsia kama nguzo ya kuimarisha demokrasia, sheria haijabainisha uwajibikaji wa vyama vya siasa katika kutekeleza msingi huu katika uongozi wa vyama husika na wa uteuzi wa wagombea

d) Vilevile, Wizara na taasisi zake zipitie kanuni zinazoongoza mwenendo wa uchaguzi. Kwa mfano, Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani 2015. Miongozo na maadili husika havikubainisha miongozo ya kuwawajibisha wasiozingatia maadili yanayohusu ukiukwaji wa haki za msingi za wanawake katika mchakato mzima wa uchaguzi.

Sisi Wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozi na mitandao mingine ya Tapo la ukombozi wa wanawake, tunatoa wito kwa wizara ya Sheria na Katiba ikiongozwa na Tume ya Kurekebisha Sheria ichukue hatua stahiki katika kipindi hiki cha maandalizi kupitia upya sheria na miongozi husika, ili kuleta maboresho yatakayozingatia mapengo ya kijinsia yatakayobainishwa.

### 3.1.3 TUME YA UCHAGUZI

Tume ya uchaguzi imepewa dhamana kubwa ya kuratibu shughuli zote za mchakato wa uchaguzi, hivyo ina wajibu wa kusimamia misingi ya haki, usawa, utawala bora katika kuteua wasimamizi wa uchaguzi, kubainisha mipaka na majimbo ya uchaguzi, kusimamia elimu ya uraia yenye kuzingatia misingi ya usawa wa jinsia na demokrasia thabiti, kusimamia zoezi lote la uchaguzi kabla ya uchaguzi, wakati wa kupiga kura na hatimaye baada ya kupiga kura. Kutoa ripoti yenye kuonesha mafanikio, changamoto na mafunzo ikibainisha masuala ya jinsia wakati wa mchakato wote katika majukumu yake. Sisi Wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozi na mitandao mingine ya Tapo la ukombozi wa wanawake, tuna madai haya kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi:

**Madai kwa Tume ya Uchaguzi**

a) Tume ya Uchaguzi ihakikishe watendaji wake wote wanaelimishwa kuhusu haki za wanawake katika uchaguzi kama zilivyobainishwa katika mikataba ya Kimataifa na ya Kikanda, pamoja na Katiba ya nchi.

b) Tume ya Uchaguzi katika kuratibu zoezi la uandikishaji wa wapiga kura, ihakikishe imeweka mazingira wezeshi kwa wanawake kufikia vituo vya kujiandikisha pamoja na kuwezesha wazingatie muda, na umbali, ili wanawake waweze kufikia vituo na kupata maelezo sahihi kuhusu uandikishwaji wao kwenye daftari la wapigakura. Elimu ya kutosha itolewe na Tume ikishirikiana na asasi za kiraia kuhusu umuhimu wa kujiandikisha.

c) Tume izingatie haki za wanawake wenye changamoto mbalimbali kama za macho, kusikia, kufikia huduma, na hata wanawake wenye

ujauzito. Tume ihakikishe wanawake hawa hawanyimwi haki zao za kujiandikisha, za kupata elimu ya wapigakura, kuteuliwa, kupiga kura, na hata kuonesha kwenye ripoti ya uchaguzi changamoto walizopitia kwenye kipindi chote cha uchaguzi ili kupata mafunzo ya kurekebisha katika chaguzi nyingine.

d) Tume izingatie usawa wa kijinsia katika kuteua watendaji wakuu kwenye zoezi lote la uchaguzi.

e) Kwenye utoaji wa elimu ya mpigakura, Tume ihakikishe imeingiza masuala ya haki za wanawake katika elimu hiyo ikishirikiana na asasi za kiraia hususani zile zinazotetea haki za wanawake.

f) Kwenye uratibu wa kampeni, Tume ihakikishe imetoa ratiba rafiki kwa wagombea wanawake na kuhakikisha kwamba wagombea wote wanawake wana fursa ya kunadi sera zao.

g) Tume isimamie zoezi la kampeni na kukemea pamoja na kuchukua hatua stahiki dhidi ya wagombea wanaowadhalilisha wanawake.

h) Kwenye kuelimisha wachunguzi wa Uchaguzi, Tume ihakikishe imewaelimisha kuhusu masuala ya jinsia kwenye mchakato ikiwa ni pamoja na uchunguzi wa vitendo vinavyowadhalilisha wanawake.

i) Kwenye usimamizi wa kupiga kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo, Tume ihakikishe usalama wa wanawake wapigakura, waliowania uchaguzi na hata wale wanaosimamia uchaguzi.

j) Mwisho, japo si kwa umuhimu, Tume inapotayarisha ripoti ya mchakato mzima wa uchaguzi ihakikishe imebainisha masuala ya jinsia katika mchakato wote ili ripoti husika itoe mafunzo kwa mchakato utakaofuata.

### 3.1.4 TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA (TAKUKURU)

TAKUKURU ni taasisi ya umma iliyopewa dhamana ya kusimamia na kufuatilia utendajikazi wa mifumo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mfumo wa uchaguzi kwa ajili ya kubaini mianya ya rushwa. Ripoti za wasimamizi na wachunguzi wa chaguzi za mitaa na zile za Urais na Wabunge, zilizopita zimebaini kuwapo kwa viashiria vya rushwa ya ngono katika chaguzi zote. Hata hivyo, eneo hili huwa haliko wazi kwani wahanga husita kutoa taarifa, hasa pale ambapo walilazimika kutoa rushwa ili wateuliwe, au wapewe wadhifa fulani kwenye mchakato wa uchaguzi. Hivyo basi, kwa kutambua ukubwa wa tatizo hili, Sisi Wanawake, Wanamtandao wa Katiba, Uchaguzi na Uongozi na mitandao mingine ya Tapo la ukombozi wa wanawake, tunadai mambo ya fuatayo kwa TAKUKURU.

#### Madai kwa TAKUKURU

a) Katika jukumu la kuelimisha raia kuhusu suala la rushwa hususani rushwa ya ngono, TAKUKURU ishirikiane na asasi za kiraia kuelimisha umma kuhusu athari za rushwa ya ngono kwenye kudhalilisha utu wa mwathirika, kwenye ukiukwaji wa haki zake za msingi hasa pale anapolazimika kubadilisha ngono kwa kupata haki zake, kama uteuzi ndani ya chama.

b) TAKUKURU ikishirikiana na asasi za kiraia iwajengee uwezo wanawake wanaowania nafasi mbalimbali kwenye uchaguzi ili wawe na uthubutu wa kuwataja wale wote wanaowashawishi kubadilisha haki zao kwa ngono, ili kuvunja ukimya ulioko kwenye changamoto hii.

c) TAKUKURU ihakikishe kwamba vitendo vyote vya rushwa pamoja na rushwa ya ngono vinachukuliwa hatua stahiki ikiwa ni pamoja na hatua za kimahakama kama zilivyoainishwa kwenye sheria husika.

### 3.1.5 Vyombo vyote Vinavyosimamia Haki na Utawala wa Sheria kwenye Uchaguzi (Polisi na Tume ya Haki za Binadamu).

Kesi zitokanazo na uchaguzi zinahitaji gharama kubwa ambazo wanawake wengi hawawezi kuzimudu. Kwa sababu hiyo, sisi Wanawake wa Mtandao wa Katiba, Uongozi na Uchaguzi na mitandao mingine ya Tapo la ukombozi wa wanawake tuna madai haya kwa mahakama na wale wote wanaosimamia utoaji wa haki wakati wote wa zoezi la uchaguzi.

**Madai kwa Mahakama na Taasisi zinazoshughulikia Haki za Binadamu**

a) Wanawake wengi wagombea na hata wapigakura watakuwa na uhitaji mkubwa wa msaada wa kisheria ili waweze kutoa malalamiko yao bila vitisho.

b) Kesi zinazohusu rushwa ya ngono zinahitaji ufaragha mkubwa ili wahanga wawe huru kujieleza na kujitetea. Mahakama ihakikishe ulinzi wa wanawake wenye kutoa malalamiko yao mahakamani.

c) Jeshi la Polisi lina nafasi kubwa sana katika kuwawezesha wanawake kupata haki zao pale zinapokiukwa. Tunalitaka jeshi hili liharakishe kupokea na kupeleka mahakamani malalamiko ya wanawake, wawe wapigakura, waliowania nafasi za uteuzi ndani ya vyama vyao, au wale wanaogombea uteuzi katika nafasi mbalimbali.

d) Tume ya Haki za Binadamu zisimamie utekelezaji wa maadili na ukiukwaji wa haki za wanawake katika uchaguzi.

Sisi Wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozi na mitandao mingine ya Tapo la ukombozi wa wanawake tuseme kwa sauti moja kwamba, ucheleweshwaji wa haki, ni sawasawa na unyimwaji wa haki

### 3.1.6 Madai kwa Msajili wa Vyama vya Siasa

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ina wajibu wa kusimamia uzingatiaji wa sheria ya Vyama vya Siasa kama kwenye utekelezaji wa majukumu ya vyama kwa kuzingatia msingi ya usawa wa kijinsia.

Kwa mantiki hii, Sisi Wanamtandao wa Wanawake Katiba Uchaguzi na Uongozi na mitandao mingine ya Tapo la ukombozi wa wanawake tuna madai haya kwa ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

a) Msajili wa Vyama vya Siasa kuhakikisha kila chama kilichosajiliwa na kinachoshiriki katika chaguzi hizi mbili, kinazingatia usawa wa jinsia katika (a) kutayarisha na kutekeleza sera za vyama (b) uteuzi wa wagombea wa nafasi za uongozi katika chaguzi na (c) uchaguzi wa viongozi wa vyama.

b) Kuhakikisha kwamba rasilimali za vyama wakati wa uchaguzi zinatumika katika kuwezesha wanawake kushiriki katika uchaguzi.

### 3.2 Madai kwa Vyama vya Siasa

Vyama vya siasa ni mhimili mkubwa wa demokrasia shirikishi na ya ushindani. Vilevile, vyama vya siasa ni walinzi wa Lango Kuu la kuingia katika kinyang'anyiro cha uchaguzi na hatimaye katika nafasi muhimu za uongozi wa taifa letu. Hivyo basi, sisi Wanamtandao wa Wanawake, Katiba Uongozi na Uchaguzi, tuna madai yafuatayo kwa vyama vya siasa.

a) Vyama vya siasa, vichukue hatua za makusudi kubadilisha mifumo ya uteuzi na uchaguzi wa viongozi ndani ya vyama ili kutoa fursa stahiki kwa wanachama wanawake kushiriki katika uongozi na maamuzi ndani ya vyama husika.

b) Vyama vya siasa vizingatie misingi iliyobainishwa kwenye mikataba ya kimataifa, kikanda, kwenye katiba ya nchi pamoja na Dira ya Taifa 2025 kuhusu usawa wa kijinsia kwenye uongozi ndani ya vyama husika.

c) Vyama vya siasa vijielimishe kuhusu faida ya kuzingatia usawa wa jinsia katika uongozi na maamuzi ndani ya vyama ili vione umuhimu wa kuleta mabadiliko katika mfumo wa uongzi ndani ya vyama husika.

d) Vyama vya siasa vitenge mafungu maalumu ya kuwawezesha wanawake hususani vijana kushiriki katika uongozi.

e) Vyama vya siasa viache malumbano ya ubinafsi na badala yake wajenge hoja na utamaduni wa majadiliano ya kistaarabu yasiyo na vitisho au vitendo vya kuwadhalilisha wanawake wakati wa mchakato wote wa uchaguzi.

f) Vyama vya siasa vioneshe nia kweli ya kupambana na ufisadi na rushwa za aina zozote zile ikiwa ni pamoja na rushwa ngono na ukatili wowote wa kingono.

g) Vyama vya siasa viache kutumia viti maalumu kushawishi wanawake kujiondoa kwenye nafasi za kushindana kwenye majimbo, jambo ambalo linasababisha kuendelea kutumiwa kuwapigia debe wanaume wanaowania nafasi hizo

h) Wanawake wanachama wa vyama vya siasa watambue kwamba pale wanapochaguliwa kwa mfumo wa 'Viti Maalumu' hawana

fursa sawa za ushiriki katika uongozi ndani ya vyombo walivyomo. Aidha, hawawezi kuteuliwa kwenye nafasi ya Waziri Mkuu, na katika mabaraza ya tawala za mikoa, wanawake waliyoingia kwa mfumo wa 'Viti Maalumu' hubaguliwa katika uteuzi wa wenyeviti wa kamati mbalimbali, (hata pale ambapo sheria haikatazi). Vilevile, hawastahili fedha za mfuko wa jimbo zinazowezesha wenzao kuendelea kujiimarisha kwenye majimbo yao ya uchaguzi.

Sisi Wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozi na mitandao mingine ya Tapo la ukombozi wa wanawake kwa sauti moja tunakiri kwamba hatutaunga mkono chama chochote kitakachoshindwa kuonesha mambo yafuatayo :

a) Hatutakiunga mkono chama ambacho hakioneshi nia ya dhati ya kubomoa mfumodume na mifumo kandamizi ndani ya vyama vyao inayojidhihirisha kwenye safu ya uongozi wa vyama, na safu ya waliyoteuliwa kuwania nafasi kwenye chaguzi hizi mbili.

b) Hatutakiunga mkono chama chenye viongozi wanaojulikana kudhalislisha wanawake katika ngazi yoyote tangu ngazi ya kaya. Sisi wanamtandao tunasema, kumdhalilisha mwanamke yeyote ni kutudhalilisha sisi sote.

c) Hatutaunga mkono vyama au chama chenye historia ya viongozi waliofuja mali ya taifa, na kujilimbikizia mali kwa njia zisizo halali.

d) Vilevile, hatutaunga mkono, chama/vyama visivyoonyesha utayari wa kimkakati wa kufungua milango ili wanawake washiriki kikamilifu ndani ya vyama vyao na katika kuwania uongozi wakati wa uchaguzi.

Sisi Wanamtandao wa Wanawake, Katiba, Uongozi na Uchaguzi na mitandao mingine ya Tapo la ukombozi wa wanawake kwa sauti moja tunakiri tutaunga mkono chama/vyama vilivyoteua wagombea katika nafasi mbalimbali ambao kwa maoni yetu, ni wagombea wenye kusheshimu utu wa wanawake, ambao hawana tamaa ya kuhodhi madaraka, walio tayari kusimamia na kuweka mbele maslahi ya taifa ili kuhakikisha kwamba rasilimali na utajiri wa taifa letu unatumika kwa maslahi ya watanzania. Wagombea ambao hawana historia ya ufujaji mali, wizi au kashfa za ngono au udhalilishaji wowote ule wa kijinsia.

## 3.3 Madai kwa Wagombea

Katika chaguzi zilizopita, wanaharakati wapigakura tulishuhudia baadhi ya wagombea wasio na sifa wakihaha kutumia uwezo wao wa kifedha kununua kura. Kiongozi kama huyu ni sumu kwa taifa letu, ni sumu kwa demokrasia na ni simu kali kwa harakati zote zinazolenga kuwakomboa wanawake na makundi yaliyo pembezoni yanayotaabika kutokana na rasilimali za taifa kutowafikia. Vilevile, tulishuhudia wagombea waliotumia lugha za kuwadhalilisha wagombea wengine hasa wanawake,

Sisi kwa umoja wetu tunakiri kwamba mgombea anayetumia lugha ya kudhalilisha utu wa mwanamke, ametudhalilisha sisi wanawake wote, na kwamba mgombea kama huyu amefilisika kimawazo na hastahili kura zetu. Hivyo basi, Madai yetu kwa wagombea ni haya:

a) Mgombea yeyote kamwe asitumie nguvu ya fedha kununua kura bali atumie busara na nguvu ya hoja kushawishi wapiga kura.

b) Mgombea yeyote au mpigadebe ajiepushe kutumia lugha ya matusi au kuonesha ubabe wa kumdhalilisha mwanamke yeyote anayegombea nafasi yoyote ile.

c) Mgombea asiwarubuni wananchi wanawake kwa wanaume kwa ahadi ambazo hataweza kuzitimiza kwa dhamana atakayopewa.

d) Mgombea aoneshe nia ya dhati ya jinsi atakavyojihusisha na masuala ya kuleta usawa wa kijinsia na kuyapa kipaumbele masuala kama ukatili na ubaguzi wa kijinsia

## 3.4 Madai kwa Asasi za Kiraia

Katika chaguzi zilizopita, asasi nyingi za kiraia zimejihusisha na elimu ya wapigakura, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha jamii kupiga kura, kuwachagua viongozi bora na waadilifu. Aidha, elimu ya wapigakura imetolewa siku chache tu kabla ya uchaguzi, na haikuwa endelevu. Kuna asasi chache sana zilizowekeza kwenye kutetea na kuhamasisha jamii kuhimiza wanawake wenye uwezo kujitokeza, zipo chache zilizowawezesha kwa njia ya elimu, na chache sana zilizoendeleza elimu ya wapigakura kwa muda mrefu. Jambo hili linaathiri uelewa mdogo wa wapigakura kuhusu kanuni, taratibu na haki na wajibu wao katika uchaguzi wa viongozi. Kwa mantiki hii, sisi wanaharakati wapigakura, tuna madai haya kwa asasi za kiraia hususani zile zenye kujihusisha na elimu ya uraia.

a) Asasi ziunganishe nguvu ya pamoja kwenye kuwahamasisha wanawake wenye uwezo kugombea nafasi za uongozi, kukataa kuburuzwa kama wapigadebe, na kukataa kurubuniwa na nafasi za 'upendeleo' zinazotumiwa sasa hivi kama kigezo kikuu cha kumpeleka mwanamke kwenye nafasi za uongozi iwe bungeni au halmashauri.

b) Asasi za kiraia zibuni elimu endelevu kwa wapigakura yenye kuzingatia maswala ya haki za wanawake katika uongozi wa taifa, kama sehemu muhimu ya kuendeleza demokrasia–shirirkishi.

c) Asasi za kiraia zioneshe kwa vitendo imani thabiti isiyobagua wanawake na makundi mengine katika nyanja mbalimbali za uongozi.

## 3.5 Madai ya Vyimbo vya Habari

Wakati wa uchaguzi wowote, vyombo vya habari ni mhimili mkuu unaounganisha wagombea na wapigakura, pamoja na kutoa viashiria vinavyoweza kusababisha vurugu wakati wa uchaguzi. Vilevile, vyombo vya habari vinatoa fursa na jukwaa la kujadili masuala nyeti kuhusu mustakabali wa taifa kwenye maeneo mengi ikiwa ni pamoja na masuala ya jinsia. Kwa kiasi kikubwa, vyombo vya habari huwawezesha wapigakura kufanya maamuzi mazito kuhusu nani wamchague. Kwa ufupi, vyombo vya habari vina nguvu kubwa ya kuwezesha mabadiliko ya mfumo kandamizi pale ambapo vinakemea ubaguzi, vitendo vya rushwa wakati wa uchaguzi ikiwa ni pamoja na rushwa ya ngono. Hata hivyo sisi watetezi wa haki za wanawake tumeshuhudia baadhi ya vyombo vya habari vikiacha kabisa kutoa taarifa chanya kuhusu wagombea wanawake na kuendeleza taarifa za unyanyaswaji wa wanawake wakati wa uchaguzi. Hivyo basi, madai yetu kwa vyombo vya habari ni:

a) Vyombo vya Habari, hususani vile vinavyomilikiwa na umma, vihakikishe vina mpango madhubuti unaotoa taarifa na kuelimisha umma wa Tanzania kuhusu haki za wanawake katika kushiriki kwenye chaguzi zote.

b) Vyombo vya habari vikiweko vya mtandaoni vikemee na kujiepusha na tabia za ukatili dhidi ya wanawake hususani wakati wa uchaguzi na hata baada ya uchaguzi.

c) Baraza la Habari (MCT) pamoja na vyombo vyote vinavyosimamia utoaji wa habari, vihakikishe kunakuwa na mifumo ya uwajibikaji katika kutoa taarifa ili kuhakiki matumizi mabaya ya vyombo vya habari kwenye kuwadhalilisha wanawake wagombea na hata wapigakura.

d) Vyombo vya habari na hasa vile vyenye kudai uhuru wa utoa na kupokea habari, vijihusishe zaidi na kuandika makala mbalimbali na kutayarisha vipindi maalumu vinavyolenga kuibua mjadala wa kitaifa kuhusu ushiriki wa wanawake katika mchakato wa uchaguzi na faida zake.

e) Pia, vyombo vya habari viwape wagombea wanawake kipaumbele kwenye matamko yao wakati wa kampeni, na wanahabari watoe taarifa wakati wa mchakato wote wa uchaguzi kuhusu vitendo vinayosababisha ushiriki mdogo wa wanawake katika mchakato wote wa uchaguzi.

f) Kuhakiki habari zinazoletwa kuhusu haki za wanawake na kuzipa vipaumbele zile zenye ujumbe chanya na kukemea ujumbe hasi.

g) Kuhimiza waandishi wa habari kutoa taswira chanya ya wanawake wanaowania kuchaguliwa.

h) Kuhakiki matumizi ya lugha ili kuondoa zile lugha za kudhalilisha wanawake.

i) Kuwapa wanawake wagombea nafasi ya kwanza kwenye kurasa za habari au vichwa vya habari.

j) Wanahabari wanapaswa kujielimisha kuhusu masuala ya jinsia katika mchakato wote wa uchaguzi ili kubaini mapengo ya utekelezwaji wa sheria za uchaguzi kwa mrengo wa jinsia. Maarifa haya yatawapa wanahabari nyenzo ya kutetea haki ya ushiriki wa wanawake katika mchakato wa uchaguzi.

k) Vyombo vya habari viunganishe nguvu na watetezi wa haki za wananchi hususani za wanawake katika kutetea haki zao za ushiriki kwa kutumia vyombo husika.

l) Wadau mbalimbali waunganishe nguvu ili kuwawezesha wagombea wanawake hususani vijana, kutumia vyombo vya habari katika kampeni zao.

m) Baraza la habari, na wanadau wengine wa habari, waandike ripoti ya mchakato wote wa uchaguzi itakayolenga kueleza jinsi vyombo vya habari vilivyohusika na ama jitihada za kubomoa fikra za kumdhalilisha mwanamke au vilivyoweza kushiriki kwenye kubomoa mfumo wa kifikra kuhusu ushiriki wa wanawake katika zoezi lote la uchaguzi.

## 3.6 Madai kwa Serikali Itakayokuwa Madarakani

Kwa serikali tutakayoipa dhamana ya kuendesha shughuli kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, kwa sauti moja tunadai.

Serikali itakayowekwa madarakani ihakikishe inasimamia kwa uadilifu matumizi na rasilimali ya taifa letu, ili rasilimali hii itumike kwa manufaa ya watanzania wote, wanawake kwa wanaume, watoto kwa wazee sambamba na usimamizi wa rasilimali ya taifa, ni usimamizi wa utawala bora na uwajibikaji kwa mtazamo wa jinsia.

Hivyo basi, serikali itakayopewa dhamana ya kuongoza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo sharti ifanye mambo haya :

a) Kuendeleza jitihada za kuondoa vizingiti vinavyosababisha ubaguzi dhidi ya wanawake katika sheria, sera na hata katika matumizi ya rasilimali za taifa.

b) Kuchukua hatua za makusudi za kuziba mapengo yaliyobainishwa katika uongozi, elimu, afya, uchumi na umiliki wa rasilimali za taifa hli.

c) Kuimarisha mikakati ya kuondoa ukatili dhidi ya wanawake na watoto wa kike.

d) Kubuni mikakati madhubuti ya kuwawezesha wanawake kiuchumi ili washiriki kikamilifu katika ujenzi wa Tanzania ya Viwanda, kama wamiliki, wafanyakazi kwenye ajira za kipato cha juu, na wanaonufaika na matunda ya jasho lao.

e) Kuwekeza katika mchakato wa utayarishwaji wa katiba mpya itakayozingatia madai ya wanamtandao kama yalivyobainishwa na Bunge Maalumu: Katiba Inayopendekezwa (Oktoba 2014)

f) Kukataa kuuza haki zetu kama wapigakura,

g) Kukataa kurubuniwa na watu wenye uchu wa madaraka, wenye tabia ya kuhodhi madaraka,

h) Kukataa kuendelea kuwapigia debe wakati wa uchaguzi watu wanaokumbatia mfumodume katika maisha yao ya kila siku.

i) Kudai uwakilishi wa 50/50 utakaowezeshwa na mabadiliko ya mfumo wa uchaguzi hususani wa 'Viti Maalumu' kwani haujaleta mabadiliko endelevu katika mfumo wa uchaguzi uliojengeka katika misingi ya ubaguzi wa kijinsia.

## 4. HITIMISHO

Sisi wanaharakati wa kutetea haki za wanawake, tunahitimisha Ilani hii ya Uchaguzi kwa kutamka kwa pamoja kwamba, mfumodume, kama ilivyo mifumo yote kandamizi, hauwezi ukajenga mazingira ya kidemokrasia endelevu, wala hauwezi kupunguza au kuondoa umaskini. Ushiriki wa wanawake katika ngazi zote za maamuzi ni haki yao ya kikatiba, na serikali inawajibu mkubwa sana katika kuweka mazingira yatakoyowezesha wanawake kudai haki zao, kuzitetea na kuzilinda. Vilevile, tunajua kwamba, hatima ya nchi yetu iko mikononi mwetu, tuna uwezo mkubwa sana wa kuleta mabadiliko makubwa na ya kimapinduzi katika nchi yetu endapo tutaunganisha nguvu zetu kujenga ajenda moja, sauti moja, kudai uwakilishi wa 50/50 katika chaguzi hizi mbili na kukataa mfumo wa viti maalumu.

TUTAMBUE KWAMBA KURA ZETU NI TURUFU YA USHINDI KWENYE CHAGUZI ZOZOTE NA KWAMBA, SISI KWA UMOJA WETU TUNA UWEZO, TUNA AJENDA MOJA, TUNA NIA, TUNA SABABU, NA NI HAKI YETU KULETA MABADILIKO TUNAYOYATAKA KWENYE MIFUMO INAYOTUBAGUA.

## Kwa Taarifa Zaidi

**Mtandao wa Jinsia Tanzania**
Mabibo Dar es saalam
S.L.P 8921
**Simu:** +255 754 784 050
**Barua Pepe:** info@tgnp.or.tz
**Tovuti:** www.tgnp.or.tz

@tgnptz1 @tgnptz @tvtapo
Tanzania Gender Networking Programme (TGNP)

